



Matibabu ya maambukizi ya kifua kikuu hafifu (LTBI)

Kwa nini nahitaji matibabu ya kukinga TB?

Kipimo chako chanya cha Mantoux (kipimo cha ngozi cha kifua kikuu) kinaonyesha kuwa umeathirika na wadudu wa kifua kikuu (TB) (Mycobacterium tuberculosis). X-ray yako ya kifua na vipimo vinaonyesha kuwa HUNA ugojwa wa kifua kikuu na huwezi kuambukiza vijidudu kwa mtu mwingine. Kuwa wameambukizwa au kuwa na maambukizi ya TB hafifu (LTBI) ina maana kwamba unaweza kuwa katika hatari ya kupatwa na ugonjwa huo wakati fulani katika maisha yako hasa kama ulinzi wa mwili wako ukiwa dhaifu kwa sababu yoyote. Kwa kuchukua vidonge Isoniazid (INH) kwa muda wa miezi 9, unaweza kupunguza hatari ya kuwa na ugojwa wa TB kwa mpaka asilimia 92%

Hivyo kama watu 100 wakiambukizwa (Mantoux chanya), 10 hadi 20 watakuwa na uwezekano wa kuendelea na kupata TB katika maisha yao na 5 hadi 10 ya kesi hizi za TB zitatokea ndani ya miaka 2-5 ya maambukizi. Kama watu wote 100 wenye Mantoux chanya wakitumia vidonge vya INH basi ni chini mtu 1 hadi 2 watapatwa na TB maana INH inafanyakazi kuondokana na maambukizi ya vidudu hafifu au hai.

Dawa gani naweza kutumia ili kuzuia TB?

Dozi ya miezi 9 ya INH huchukuliwa ili kuzuia ugonjwa wa TB ili usikue. INH hutolewa kulingana na uzito wako kwa watu wazima na kipimo cha kila siku kawaida ni vidonge 3 X 100mg. INH wakati mwingine hutolewa mara 3 kwa wiki, kwa kiwango cha juu (mfano 600mg Jumatatu-Jumatano-Ijumaa), kama matibabu yanayo simamiwa na mfanyakazi wa huduma za afya. Vitamini B6 ya ziada (pyridoxine) pia hutolewa ili kupunguza hatari ya kutokea madhara mabaya.

Kipimo cha damu kabla ya kuanza dawa za INH

INH mara chache inaweza kusababisha kujisikia kulewa (ini kuvimba). Kabla ya kumeza INH, ini lako litapimwa ili kuangalia kama inafanya kazi vizuri. INH haishauriwi kutumiwa na watu wenye ugonjwa wa ini au kwa wale ambao wanatunia pombe iliyokithiri. **Ni muhimu sana kuepuka / kupunguza kunywa pombe wakati ukitumia INH maana pombe huongeza hatari ya kiwango cha sumu kubwa ya ini.**

Je INH ni salama?

INH imeshatumiwa na mamilioni ya watu duniani kote na kwa ujumla ni nzuri kwa kutumiwa. Hata hivyo, kama ilivyo kwa dawa yoyote, inaweza wakati mwingine kusababisha madhara. Mwambie daktari wako, mfanyakazi wa afya wa Kiaborijino au muuguzi mara moja kama kuna dalili za magojwa zizizotarajiwa au kama mojawapo ya dalili hizi zikitoka:

- tumbo kuvurugika
- kupoteza hamu ya kula
- kichefuchefu
- kutapika
- upele / ukurutu
- ngozi ya njano
- mkojo wa rangi nyeusi (chai rangi)
- ganzi au kufa ganzi ya mikono na miguu
- homa ya kudumu siku 3 au zaidi
- utepetevu wa awali(kwa kawaida hutoweka ndani ya mwezi wa kwanza)

Uchunguza wa kila mwezi

Wakati ukiwa unatumia INH, matembezi ya kila mwezi kwenye Kliniki ya TB yanatakiwa. Lengo ya matembezi hayo ni:

- Kupimwa uzito na afya kwa ujumla
- Kupimwa madhara yoyote yatokanayo na vidonge
- Kuangalia kama unameza vidonge vizuri na kupewa dawa zingine za mwezi.

Inatokea nini kama nikisahau kumeza vidonge?

Kama kusahau kumeza vidonge vyako kwa siku moja tu, usiwe na wasiwasi. Endelea kutumia dozi yako ya kila siku siku ya pili kama kawaida. Kama ukisahau mara nyingi sana, dawa haziwezi kufanya kazi kwa ufanisi. Ni rahisi kukumbuka kumeza vidonge vyako kama ukivimeza wakati huo huo kila siku. Pia ni bora kuvimeza kabla ya kula chochote tumboni.

Ushauri wa ujumla wakati ukitumia INH

- Meza vidonge vyako vya INH angalau nusu saa kabla ya milo au wakati wa kwenda kulala.
- Meza vidonge ukitumia maji, maziwa, au glasi ya juisi.
- kula chakula cha afya na kupata mapumziko ya kutosha.
- ***Epuka kunywa pombe.***
- Mwambie daktari wako, mfanyakazi wa afya wa Aborijino au muuguzi wa TB kuhusu dawa zingine unazozitumia kabla ya kuanza dawa mpya.
- ***wanawake*** wanaotumia INH ni muhimu kuepuka ujauzito mpaka matibabu yamekamilika. Hii ni kwa sababu mimba inaweza kuongeza hatari ya madhara kuhusiana na ini. Kama una mimba toa taarifa kliniki ya TB haraka iwezekanavyo.
- Vidonge vya uzazi wa mpango vinaweza kutumiwa wakati wa ukitumia INH.

Itatokea nini kama nikisogeleana na mtu mwenye TB hai mara baada ya kumaliza dozi ya INH

Kumaliza dozi ya tiba kwa ajili ya LTBI (matibabu ya kuzuia) unaua vijidudu TB hafifu katika mwili wako. Baadaye, kama ukiambukizwa tena, hatari ya kuendelea na ugonjwa huo ni ya ndogo sana (kiasi cha robo) *. Kutibu TST yako ya awali ni muhimu sana. Hata hivyo, kama ukiambukizwa tena (Kutambulika kama umeambukizwa TB) marudio ya kliniki na X-ray ya kifua inapendekezwa.

Habari zaidi

Kwa habari zaidi wasiliana na Kliniki ya TB kwenye mkoa wako

Alice Springs 89517548

Darwin 89228804

Katherine 89739040

Nhulunbuy 89870282

Tennant Ck 89624259

au www.nt.gov.au/health/cdc

* Sutherland et al. The Development of Clinical Tuberculosis Following Infection with Tubercle bacilli. *Tubercle*. 63(1982) 255-268.